NISHATI | HABARI ZA NISHATI

# News Bulletin

www.nishati.go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

Toleo Namba 31 Oktoba 1 - 31, 2021

# MRADI WA UMEME RUSUMO KUUNGANISHA MIKOA YA KAGERA, KIGOMA, RUKWA NA KATAVI KWENYE GRIDI YA TAIFA - MAJALIWA




*Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato (wa pili kushoto) kuhusu handaki la kuchepusha maji wakati alipotembelea Mradi wa Umeme wa Rusumo wilayani Ngara , Septemba 19, 2021. Mradi huo utakaozalisha umeme kwa kutumia maji unagharimiwa na nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)*

## WATANZANIA WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA ZA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
**Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma**




## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
**Mhandisi Leonard Masanja**
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**
**Kheri Mahimbali**

**Mhariri**
**Dorina G. Makaya**

**Waandishi**
Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

**Wasiliana nasi kwa simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi:** +255-26-2320148
au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano**
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma

*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*

# Mradi wa umeme Rusumo mkombozi wa uhakika

KAULI ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kuwa mradi wa kuzalisha umeme wa kikanda wa Rusumo utakuwa mkombozi kwa wananchi wa mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa na Katavi inatia moyo na faraja kwa wakazi wa eneo hilo la nchi.

Hiyo inatokana na ukweli, kwamba mradi huo utazalisha umeme wa uhakika utakaowezesha mikoa hiyo sasa kuunganishwa na gridi ya Taifa na hivyo kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, mradi huo unaotekelezwa kwa kuzingatia makubaliano ya kiserikali ya nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi, baada ya kuingia makubaliano rasmi mwaka 2012 na utazalisha megawati 80 na kila nchi mwanachama kupata megawati 27.

Kwa kuzingatia kuwa changamoto ya umeme nchini ni kikwazo dhidi ya kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati, ikiwamo ya kuzalisha pia umeme ni dhahiri kuwa mradi huu unathibitisha kuwa mkombozi wa uhakika kiuchumi.

Watanzania chini ya uongozi wa Rais Samia, hatuna budi kuishukuru Benki ya Maendeleo ya Afrika ambayo ndiye mfadhili mkuu aliyetoa Sh bilioni 82 katika kuhakikisha kuwa mradi huo unatekelezeka kwa maslahi mapana ya nchi.

Kama ulivyo mwito kwa wakandarasi na wasimamizi wa mradi uliotolewa na Waziri Mkuu, ni vema katika utekelezaji wa mradi huo ambao kwa ujumla umefikia asilimia 81.2 ya utekelezaji, wakaongeza kasi katika ujenzi na kuepuka vikwazo ambavyo awali vilisababisha mradi huo usikamilike kwa wakati.

Ni vema ikawa hivyo kwa kuzingatia kuwa mradi huo kwa nchi zote tatu, ni sehemu ya kuendeleza uhusiano mzuri baina ya nchi hizo pamoja na kuendelea kudumisha udugu na ushirikiano.

Ni jambo la faraja pia kusikia kwa Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, kuwa mradi huo umetoa ajira 726 kwa nchi hizo tatu, Tanzania ikipata nafasi 260 za ajira, na pia utakuwa kichocheo cha uwekezaji katika sekta ya viwanda ikiwemo uzalishaji wa madini ya Nickel kwenye kata ya Bugarama, Ngara.

Kwa kuwatia moyo ni vema nchi hizi tatu zikawapongeza kwa uwazi wakandarasi wanne wa mradi ambapo wawili ni wa China ambao ni CGCOC Group Ltd na Jiangxi Water & Hydropower Construction Company Ltd (CGCOC - JWHC JV) wanaojenga bwawa la maji na miundombinu mingine.

Lakini pia na muunganiko wa wakandarasi Andritz Hydro GmbH ya Ujerumani na Andritz Hydro PVT Ltd ya India, wanaohusika na ufungaji wa mitambo ya kuzalisha na kusambaza umeme.

Juhudi hizi zinazoonyeshwa na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kushirikiana na nchi rafiki zilizotajwa hapo juu, zinalenga kuleta ukombozi wa uhakika wa kiuchumi ambao ukishakamilika utakuwa umezikomboa.

Nishati ya umeme ni kila kitu katika maendeleo ya uchumi hususan katika jamii ambazo zinaelekea katika maendeleo ya kidijitali na ya kisasa zaidi.

Endapo mradi huu utakamilika litabaki sasa ni jukumu la wananchi waishio maeneo hayo, kuulinda na kuhakikisha kweli unafanya kazi ya uzalishaji na kuondokana na hujuma ambazo zitafifisha ndoto ya wananchi wa nchi hizo tatu rafiki.

Ni hakika kuwa hivi sasa hasa chini ya uongozi wa Waziri Januari Makamba, miradi mingi itafanyika na kufanikiwa hususan katika sekta ya nishati ya umeme ambao ndio unategemewa kwa kiasi kikubwa hata katika kuendesha reli ya kisasa (SGR).

# MRADI WA UMEME RUSUMO KUUNGANISHA MIKOA YA KAGERA, KIGOMA, RUKWA NA KATAVI KWENYE GRIDI YA TAIFA - MAJALIWA

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amesema mradi wa kuzalisha umeme wa kikanda wa Rusumo utakuwa mkombozi kwa wananchi wa mikoa ya Kagera, Kigoma , Rukwa na Katavi kwani utazalisha umeme wa uhakika utakaowezesha Mikoa hiyo kuunganishwa na gridi ya taifa.

Mradi huo unaotekelezwa kwa kuzingatia makubaliano ya Kiserikali ya nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi baada ya kuingia makubaliano rasmi mwaka 2012 na utazalisha Megawati 80 ambao kila Nchi mwanachama atapata Megawati 27.

"Mkakati wa Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ni kuunganisha Mikoa yote kwenye gridi ya taifa, na sasa tumebakiwa na Mikoa minne ya Kagera, Kigoma, Katavi na Rukwa, huko kote kazi ya ujenzi wa laini za umeme ili kuiunganisha Mikoa hiyo unaendelea."



*Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato (wa pili kushoto) kuhusu handaki la kuchepusha maji wakati alipotembelea Mradi wa Umeme wa Rusumo wilayani Ngara , Septemba 19, 2021. Mradi huo utakaozalisha umeme kwa kutumia maji unagharimiwa na nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)*

Alisema na kuongeza.

Waziri Mkuu amesema Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia imedhamiria kuondoa changamoto ya umeme nchini kwa kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya kuzalisha umeme pamoja na kuongeza vyanzo vya kuzalisha nishati hiyo ili kuhakikisha maeneo yote ya nchini yanapata umeme wa uhakika hususan maeneo ya vijijini.

Ameyasema hayo, Jumapili, Septemba 19, 2021) baada ya kukagua mradi huo wa uzalishaji wa umeme ulioko katika eneo Rusumo Wilayani Ngara Mkoani Kagera unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa gharama ya shilingi bilioni 82.

"Nimefarijika kwa hatua iliyofikiwa na kwamba kazi bado inaendelea, hatua mliyoifikia ni nzuri, inawezekana Mheshimiwa Rais Samia nae akaja kuona maendeleo ya mradi huu ili kuendelea kuwatia moyo na kuweka mkazo katika ukamilishaji wake." Alisema

Waziri Mkuu ametoa wito kwa wakandarasi na wasimamizi wa mradi huo ambao hadi kufikia mwezi Julai, utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 81.2 ya utekelezaji kuongeza kasi katika ujenzi na kuepuka vikwazo ambavyo

# MRADI WA UMEME RUSUMO KUUNGANISHA MIKOA YA KAGERA, KIGOMA, RUKWA NA KATAVI KWENYE GRIDI YA TAIFA - MAJALIWA

awali vilisababisha mradi huo kukamilika kwa wakati. "Kwa niaba ya Mheshimiwa Rais ninapenda kutoa shukrani kwa wakandarasi na wasimamizi wote wa mradi huu".

Aidha, Waziri Mkuu amesema utekelezaji wa mradi huo kwa Nchi zote tatu ni sehemu ya kuendeleza mahusiano mazuri baina ya Nchi hizo pamoja na kuendelea kudumisha undugu na ushirikiano, "Tanzania, Burundi na Rwanda ni Nchi rafiki na zimejenga ushirikiano wa muda mrefu na sisi sote ni ndugu na mradi huu unaendelea kuthibitisha undugu wetu, hivyo ni vyema tuendelee kuenzi Uhusiano huu." Alisema.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Stephen Byabato amesema mradi huo umetoa ajira 726 kwa Nchi zote tatu na Tanzania imepata nafasi 260 za ajira, na pia utakuwa ni kichocheo cha kuwepo kwa wawekezaji katika sekta ya viwanda ikiwemo uzalishaji wa madini ya Nickel kata ya Bugarama, Wilayani Ngara.

Mradi huo unatekelezwa kwa Muungano wa Wakandarasi wanne ambapo wawili kutoka China, CGCOC Group Ltd na Jiangxi Water & Hydropower Construction Company Ltd (CGCOC - JWHC JV) wanajenga bwawa la maji pamoja na miundombinu mingine; na muunganiko wa Wakandarasi Andritz Hydro GmbH ya Ujerumani na Andritz Hydro PVT Ltd ya India wanaohusika na ufungaji wa mitambo ya kuzalisha na kusambaza umeme.



*Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitoa maelekezo kutoka kwa Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato (kushoto) kuhusu ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Rusumo wilayani Ngara, Septemba 19, 2021. Mradi huo utakaozalisha umeme kwa kutumia maji unagharimiwa na nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda( (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)*

# WATANZANIA WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA ZA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI



*Waziri wa Nishati Mhe. January Yusuf Makamba, akizungumza na Waandishi wa Habari mara baada ya kufanya ufunguzi wa kongamano la kujadili fursa na mahitaji ya Mradi kati ya wadau wa Sekta Binafsi na kampuni zitakazojenga Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) lililofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam tarehe 23 Septemba, 2021.*

**Na Dorina G. Makaya na Ebeneza Mollel Dar-es-salaam.**

Waziri wa Nishati, Mhe. January Yusuf Makamba, amewataka watanzania kuchangamkia fursa zitakazotokana na ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga, Tanzania ili kujiongezea kipato na utaalam kwani sehemu kubwa ya bomba linapita nchini Tanzania.

Waziri Makamba ameyasema hayo tarehe 23 Septemba, 2021 wakati wa ufunguzi wa kongamano la wadau wa Sekta Binafsi na kampuni zitakazojenga Mradi wa Bomba la Mafuta lililofanyika katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar es salaam.

Waziri Makamba alisema, mradi huo ni mradi muhimu kwa Tanzania, kwani ni mradi unaosafirisha mafuta kutoka Uganda mpaka Tanga na kuwa asilimia 80 ya bomba la mafuta litajengwa upande wa Tanzania na hivyo watanzania wanahimizwa kuwa tayari kutumia fursa zitakazotokana na utekelezaji wa Mradi huo.

"Hii inaonesha ni jinsi gani uchumi wa Tanzania utanufaika na mradi huu" alisema Waziri Makamba.

"Mathalani, inakadiriwa katika kipindi cha ujenzi zitatolewa takribani ajira 10,000 na pia katika kipindi cha uendeshaji zitatolewa takribani ajira 1,000 kwa Watanzania. Hivyo, ni matumaini yangu kuwa washiriki wote ikiwemo Sekta Binafsi itajipanga kikamilifu kutumia fursa hii na kuhakikisha kuwa, yale maeneo ambayo huduma zinaweza kupatikana ndani ya nchi basi fursa hizo zitolewe kwa watanzania.' Aliongeza Waziri Makamba.

Waziri Makamba alibainisha kuwa, mnamo tarehe 20 Mei, 2021, Serikali ilisaini Mkataba wa Msingi wa Mradi (Host Government Agreement [HGA]) kati yake na Mwekezaji, Kampuni ya EACOP ambapo, kupitia Mkataba huu umeainisha baadhi ya huduma na bidhaa zitakazotolewa na Watanzania pekee ikiwemo huduma za usafirishaji, ulinzi, chakula na vinywaji, huduma za malazi na usambazaji wa mafuta kwa ajili ya magari na mitambo. Amezitaja huduma nyingine kuwa ni pamoja na shajala, bidhaa za ujenzi zinazopatikana

# WATANZANIA WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA ZA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI

hapa nchini, shughuli za ujenzi, huduma za mawasiliano na ukodishaji wa mitambo ya ujenzi.

Aidha, Waziri Makamba alibainisha kuwa, bidhaa na huduma nyingine za manunuzi tofauti na zile zilizotengwa kwa Watanzania zitapatikana kwa njia ya ushindani wa kimataifa na Watanzania wenye uwezo, vigezo na sifa stahiki wajitokeze kushiriki.

Alisema, Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015, inasisitiza ushiriki wa watanzania katika miradi ya nishati inayotekelezwa nchini.

Waziri Makamba alieleza kuwa, mradi huu ni wa kimkakati na wa kihistoria utakaotoa fursa nyingi na utagharimu takriban shilingi trilioni 8.

Akizungumzia kuhusu lengo la kongamano, Waziri Makamba alisema, kongamano hilo limelenga kuzikutanisha kampuni zilizoshinda zabuni mbalimbali za ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta na wadau wa sekta binafsi nchini ili waweze kueleza mahitaji yao na utaratibu utakaokuwepo kwa watanzania kuweza kushiriki kutoa huduma mbalimbali wakati wa ujenzi wa mradi. Pia, kuwa na fursa ya majadiliano ya pamoja jinsi ya kufanya maandalizi muhimu ili kufikia matarajio ya wakandarasi wa mradi.

Waziri Makamba alieleza kuwa, Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi wa Afrika Mashariki (EACOP) utahusisha ujenzi wa Bomba la Mafuta lenye urefu wa kilomita 1,443 kutoka Hoima - Uganda hadi Chongoleni Tanga.

Waziri Makamba alieleza kuwa, Kati ya kilomita 1,443 zitakazojengwa, kilometa 1,147 ziko upande wa Tanzania na kilometa 296 upande wa Uganda.

Aidha, mradi utahusisha ujenzi wa Kambi 18 ambapo kati ya hizo, kambi 14 ziko upande wa Tanzania na 4 zipo upande Uganda.  Pia, eneo litakalotumika kujenga Coating yard litakuwa wilayani Nzega, Tabora; Vituo 6 vya kusukuma Mafuta ambapo vituo 4 vitajengwa Tanzania na vituo 2 vitajengwa Uganda.

Vile vile. Waziri Makamba alibainisha kuwa, Vituo 2 vya kupunguza kasi ya Mafuta vitajengwa Tanzania na Matanki manne (4) yenye Ujazo wa Mapipa 500,000 kila moja yatajengwa katika eneo la Chongoleani, Tanga pamoja na ghati la kupakia mafuta kwenye meli lenye urefu wa kilometa 1.9.

Akizungumzia kuhusu fidia kwa wananchi watakaopisha Mradi, Waziri Makamba alisema, hadi sasa, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya EACOP, tayari imelipa Jumla ya shilingi 2,286,540,906 kwa wananchi 351 kama fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa Kambi 14 za mradi na hivyo maeneo yapo tayari kwa kuanza




*Waziri wa Nishati Mhe. January Yusuf Makamba, akizungumza na washiriki wa  kongamano la kujadili fursa na mahitaji ya Mradi kati ya wadau wa Sekta Binafsi na kampuni zitakazojenga Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam tarehe 23 Septemba, 2021.*

# WATANZANIA WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA ZA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI



*Washiriki wa kongamano la kujadili fursa na mahitaji ya Mradi kati ya wadau wa Sekta Binafsi na kampuni zitakazojenga Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) lililofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifia wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam tarehe 23 Septemba, 2021, wakifuatilia kwa umakini hotuba iliyokuwa ikitolewa na Waziri wa Nishati Mhe. January Yusuph Makamba. (Hayumo Pichani) wakati wa ufunguzi wa Kongamano hilo.*

utekelezaji wa mradi.

Alisema, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 259.96 sawa na dola za marekani milioni 112 ikiwa ni mchango wake katika kushiriki kwenye Mradi. Aidha, Waziri Makamba ameongeza kuwa, Tarehe 30 Juni, 2021 Serikali kupitia Bunge la Jumhuri ya Muungano wa Tanzania ilipitisha Sheria ya mabadiliko ya sheria mbalimbali kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwemo mradi wa EACOP.

Waziri Makamba alitoa rai kwa Kampuni ya EACOP na washirika wake kuharakisha mchakato wa manunuzi na kuanza rasmi ujenzi wa mradi mwezi Oktoba, 2021 kama ilivyopangwa.

Aidha, alieleza kuwa, serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuwajengea watanzania uwezo stahiki ili waweze kushiriki kikamilifu katika mradi wa EACOP na miradi mingine ya kimkakati.

Waziri Makamba aliipongeza Serikali, Shirika la Maendeleo ya Mafuta Nchini (TPDC), Kampuni inayoendesha mradi wa bomba (EACOP) na Sekta Binafsi, kwa kuratibu maandalizi ya kongamano hilo na kueleza kuwa, Serikali itaendelea kufanya uelimishaji juu ya fursa za mradi kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya na vijiji pamoja na kuandaa makongamano mbalimbali.

Aidha, aliongeza kuwa, Serikali itaendelea kushirikiana na Kampuni ya EACOP kuratibu makongamano ya Wadau kwa lengo la kupeana taarifa ya utekelezaji wa mradi na kujadili fursa na mahitaji ya Mradi kwa ujumla ili kuwawezesha watanzania na wadau wote kiujumla kufahamu fursa kwa upana wake na jinsi gani waweze kujiandaa na kushiriki ipasavyo.

Mkutano huo wa wadau wa bomba la mafuta, ulihudhuriwa na viongozi mbali mbali wakiwemo Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Seif Gulamali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Leonard Masanja, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, Mwenyekiti wa Bodi ya TPDC, Halfani Halfani, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio, Mkurugenzi Mkuu Kampuni ya EACOP, Bw. Matin Tiffen, Wakurugenzi wa Taasisi na Wenyeviti wa Taasisi za Sekta Binafsi.

# WATANZANIA WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA ZA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI









*Matukio mbalimbali katika picha wakati wa kujadili fursa na mahitaji ya Mradi kati ya wadau wa Sekta Binafsi na Kampuni zitakazojenga Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) lililofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifia wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam tarehe 23 Septemba, 2021.*

# WATANZANIA WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA ZA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI













*Matukio mbalimbali katika picha wakati wa kujadili fursa na mahitaji ya Mradi kati ya wadau wa Sekta Binafsi na Kampuni zitakazojenga Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) lililofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifia wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam tarehe 23 Septemba, 2021.*

# WAZIRI MAKAMBA; WAKUU WA MIKOA WANA JUKUMU KUBWA MRADI WA EACOP



*Waziri wa Nishati January Makamba akizungumza na Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane ambayo itapitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga wakati wa semina kuhusu fursa zitakazopatikana kutokana na Mradi huo, inayoendelea jijini Tanga tarehe 27 hadi 29 Septemba, 2021.*

**Na Dorina G. Makaya na Janeth Mesomapya - Tanga.**

Waziri wa Nishati, Mh. January Yusuf Makamba ameeleza kuwa Wakuu wa Mikoa minane (8) ambapo utapita mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) wanajukumu kubwa katika kufanikisha utekelezaji wa mradi huo kwa kuimarisha ulinzi na usalama pamoja na kuhakikisha fursa zitakazopatikana zinanufaisha wananchi wa mikoa yao husika.

Waziri Makamba ameyasema hayo leo, Septemba 27, 2021 wakati wa semina kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane itakayopitiwa na mradi huo, inayofanyika jijini Tanga.

"Moja ya sababu za bomba hili kupita nchini kwetu ni uhakika wa ulinzi na usalama uliopo. Usalama huo utaendelea kuwepo kama wanaosimamia usalama huo kwenye maeneo linapopita bomba wana uelewa kuhusu mradi na kile kinachohitajika kufanywa ili walioamua bomba hili lipitie kwetu



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza na Wakuu wa mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane ambayo itapitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga, kuhusu umuhimu wa kutengeneza mazingira mazuri ili kupata fursa zitakazotokana na utekelezaji wa Mradi huo, wakati wa semina, inayoendelea jijini Tanga tarehe 27 hadi 29 Septemba, 2021*

# WAZIRI MAKAMBA; WAKUU WA MIKOA WANA JUKUMU KUBWA MRADI WA EACOP



*Mkuu wa Mkoa wa Tanga Adam Malima akiwakaribisha Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa minane ambayo itapitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga wakati wa semina kuhusu fursa zitakazopatikana kutokana na Mradi huo, inayoendelea jijini Tanga tarehe 27 hadi 29 Septemba, 2021.*

wawe na imani kwamba walifanya uamuzi sahihi", alisema Waziri Makamba.

Ameongeza kuwa semina hiyo inalenga kutengeneza uelewa mpana kwa viongozi hao kuhusu mradi na kujadili fursa mbalimbali zitakazopatikana kwenye utekelezaji wake.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato ametoa rai kwa viongozi hao kuhakikisha wanatengeneza mazingira mazuri ili fursa zitakazotokana na utekelezaji wa mradi huo zinufaishe wananchi wa mikoa husika.

Mh. Byabato amesema kuwa Bomba hilo litapita katika mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga,Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga.

Ameeleza kuwa Mkataba Hodhi wa Mradi (HGA) baina ya Serikali na Kampuni ya Bomba umeainisha baadhi ya bidhaa na huduma zitakazotolewe na Watanzania pekee (Reserved Contracts).

Naibu Waziri Byabato ameongeza kuwa, bidhaa na huduma hizo ni pamoja na usafirishaji, ulinzi, chakula na vinywaji, huduma ya malazi, mafuta kwa ajili ya magari na mitambo, shajala, bidhaa za ujenzi zinazopatikana hapa nchini, shughuli za ujenzi (civil works), huduma za mawasiliano, na ukodishaji wa mitambo ya ujenzi.

Bidhaa na huduma nyingine za manunuzi tofauti na zile zilizotengwa kwa Watanzania tu zitapatikana kwa njia ya ushindani na Watanzania wenye uwezo, vigezo na sifa stahiki wataweza kushiriki.

Ameongeza kuwa bidhaa na huduma nyingine za manunuzi tofauti na zile zilizotengwa kwa Watanzania tu zitapatikana kwa njia ya ushindani na Watanzania wenye uwezo, vigezo na sifa stahiki wataweza kushiriki.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) Dkt. James Mataragio ameeleza kuwa serikali kupitia shirika hilo inamiliki hisa asilimia 15% ya utekelezwaji wa mradi huo, huku asilimia 62% ikishikiliwa na kampuni ya Total Energies, asilimia 15% ya UNOC ya Uganda huku CNOOC ikishikilia asilimia 8%.

"Majukumu ya TPDC kwenye mradi huu ni pamoja na kuwa mbia kwenye mradi wenyewe, kushughulikia masuala ya ardhi, kusimamia mikataba yote ya EACOP, kuwa na uwakilishi wa asilimia 15% kwenye uongozi na kuwa na mjumbe kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya EACOP pamoja na kuratibu ushirikishwaji wa wadau mbalimbali watakaofanikisha utekelezaji wa mradi huu", aliongeza.

Semina hiyo iliyowakutanidha wakuu wa mikoa minane jijini Tanga pamoja na baadhi ya viongozi wa Serikali, Bunge, Wizara ya Nishati na Taasisi zake itafanyika kwa siku tatu hadi tarehe 29 Septemba, 2021.

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI YARIDHISHWA NA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UMEME WA RUSUMO

**Na Dorina G. Makaya – Kagera, Rusumo.**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeelezea kuridhishwa kwake na hatua mbalimbali za ujenzi wa Mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo MW 80 unaotekelezwa kwa kuzingatia makubaliano ya Kiserikali ya nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi ambapo kila nchi itapata MW 27.

Kauli hiyo imetolewa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Seif Gulamali, kufuatia ziara ya kamati hiyo kwenye mradi huo tarehe 12 Septemba, 2021.



*Aliyekuwa Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na Waandishi wa Habari (Hawamo pichani) wakati wa majumuisho ya ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipotembelea mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo MW 80 uliopo wilayani Ngara mkoani Kagera tarehe 12/09/2021.*

Alisema, tumejionea na kuridhika na hatua mbalimbali za ujenzi zilizofikiwa, lakini pia tumeona kuna fursa za ajira kwa watanzania na kwa nchi za Rwanda na Burundi.

Makamu mwenyekiti huyo wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, amewaomba wadau wa maeneo ya Ngara, waweze kuulinda mradi huo wa kimkakati.

"Mradi ni wa kwetu, unapoharibika mradi huu maana yake tunajiumiza sisi wenyewe kama watanzania. Kwa hiyo tuulinde mradi huu. Alisema Gulamali.

Makamu Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa, zaidi ya asilimia 75 ya mradi umejengwa katika ardhi ya Tanzania kwa hiyo ni kama mradi ni wa Tanzania hivyo uchukuliwe kwa uzito wake.

Akizungumzia kuhusu baadhi ya mapungufu yaliyobainika, Gulamali ameitaka TANESCO kulifanyia kazi suala zima la malipo ya fidia, kuyahakiki ili usitumike mwanya wa fedha za fidia kulipwa wasiostahili.



*Makamu mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Seif Gulamali akitoa ushauri kwa Serikali kuhusu utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo MW 80 uliopo wilayani Ngara mkoani Kagera, wakati kamati hiyo ilipotembelea mradi huo tarehe 12/09/2021.*



*Aliyekuwa Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akiwaonyesha wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini milango ya kudhibiti maji katika eneo la mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo MW 80 uliopo wilayani Ngara mkoani Kagera tarehe 12/09/2021.*

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI YARIDHISHWA NA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UMEME WA RUSUMO

Aliweka bayana kuwa, kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeelekeza kuwa, fidia ilipwe kwa watu waliohakikiwa, na baada ya kujiridhisha wanaostahili walipwe haki zao. Aidha, ametahadharisha kuhusu tabia ya kuibuka kwa wadai fidia wengine wanaojitokeza baada ya wahusika kulipwa fidia.

Gulamali ameiomba Serikali ya mkoa wa Kagera na Wilaya ya Ngara wasimamie kwa umakini sana mradi wa umeme wa Rusumo ikiwa ni pamoja na kuulinda kuepuka wavamizi kwenye eneo la mradi.

Akizungumzia kuhusu ukosefu wa zimamoto panapotokea majanga ya moto, Gulamali ameiomba wizara na serikali kwa ujumla Kuhakikisha gari na vifaa vya zimamoto vinapatikana na kuwepo katika eneo la mradi ili kuulinda mradi na maisha ya watu.

Awali, mbunge wa jimbo la Ngara Ndaisaba Ruhoro, aliieleza kamati ya bunge kuhusu malalamiko ya wananchi wa wilaya ya Ngara kutokulipwa fidia zao na pia kuhusu ukosefu wa zimamoto katika eneo la mradi.

Akizungumza wakati wa majumuisho, aliyekuwa Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani aliwahakikishia wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuwa Wizara ya Nishati itasimamia usiku na mchana ili kuhakikisha mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo MW 80 unakamilika kwa wakati ifikapo mwezi Desemba mwaka huu.

Alisema, kukamilika



*Baadhi ya washiriki wa Kongamano la kujadili fursa na mahitaji ya Mradi kati ya wadau wa Sekta Binafsi na kampuni zitakazojenga Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ( EACOP) lililofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar-es-Salaam tarehe 23 Septemba, 2021.*



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiongozwa na Makamu mwenyekiti wake Seif Gulamali, aliyekuwa Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani pamoja na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, wakipata maelezo kutoka kwa mmoja wa wataalam wanaotekeleza mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo MW 80 uliopo wilayani Ngara mkoani Kagera , wakati Kamati hiyo ilipotembelea mradi huo tarehe 12/09/2021.*



*Muonekano wa milango ya kudhibiti maji katika eneo la mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo MW 80 uliopo wilayani Ngara mkoani Kagera.*

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI YARIDHISHWA NA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UMEME WA RUSUMO



*Aliyekuwa Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (wa pili kutoka kulia) Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa kwanza kulia), Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Seif Gulamali wa tatu kutoka kulia, na Mbunge wa Jimbo la Ngara, Ndaisaba Ruhoro, pamoja na wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini (hawamo.pichani) wakipata maelezo kuhusu utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo MW 80 uliopo wilayani Ngara mkoani Kagera kutoka kwa Bw. Nuru Ndile, mjumbe wa bodi ya kampuni inayosimamia mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo MW 80 uliopo wilayani Ngara mkoani Kagera ambaye pia ni Kamishna Msaidizi, Idara ya Usimamizi wa Madeni Wizara ya Fedha na Mipango tarehe 12/09/2021*

kwa mradi huo, kutatatua kero ya tatizo la umeme na kuhakikisha kuna upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa bei nafuu katika mkoa wa Kagera na kuimarisha upatikanaji wa umeme mkoani Kigoma na Katavi

Mradi wa umeme wa Rusumo unatekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 340 sawa na takriban shilingi bilioni 816, mkopo wa masharti nafuu kutoka benki ya dunia (WB) na utakapokamilika utazalisha MW 80 na kila nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi zitapata MW 27 kufuatia makubaliano ya kiserikali yaliyoingiwa mwaka 2012.



*Aliyekuwa Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akitolea ufafanuzi baadhi ya hoja zilizoibuliwa katika kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakati ilipofanya ziara katika mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo MW 80 uliopo wilayani Ngara mkoani Kagera , tarehe 12 /09/2021. kushoto kwake ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Seif Gulamali na kulia kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*



*Mbunge wa Jimbo la Ngara Ndaisaba Ruhoro (aliyesimama), akiwasilisha hoja za wananchi wa Wilaya ya Ngara kuhusu madai ya fidia kwa wananchi walioathirika kutokana na utekelezaji wa Mradi wa kufua umeme wa Rusumo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipotembelea eneo la Rusumo kuona maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo wa kimkakati tarehe 12/09/2021.*

# MAKAMBA AJA NA MWELEKEO MPYA NISHATI



*Balozi wa Uingereza nchini, Donald Concar akizungumza na Waziri wa Nishati, January Makamba.*

**Na Dorina Makaya & Janeth Mesomapya**

NISHATI ya umeme ni muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Taifa lolote lile, na hivyo ili kujihakikishia maendeleo hayo, ni vema kujizatiti kwa kuwa na uhakika wa nishati hiyo.

Waziri wa Nishati, January Makamba analijua hilo na ndiyo sababu katika dhamana aliyonayo hivi sasa, ameamua kwa dhati kabisa kuhakikisha umeme haukatikikatiki na hivyo kuwezesha uhakika wa uzalishaji mali.

Amebainisha hayo baada ya kukutana na ujumbe wa Uingereza ulioongozwa na Balozi wa nchi hiyo, David Concar ukitaka kujua kuhusu utekelezaji na uwekezaji katika nishati jadidifu na hatua iliyofikiwa.

Ni kawaida kwamba kila anapoingia waziri mpya katika Wizara, mabalozi wanaowakilisha nchi zao huwa na shauku ya kutaka kujua vipaumbele vya Waziri katika sekta husika.

Ndivyo ilivyokuwa kwa Waziri Makamba katika sekta ya nishati ikiwamo gesi.

Akizungumza na Balozi Concar, Waziri Makamba alisema, katika upande wa nishati Wizara yake ilikuwa awali imejikita kwenye umeme wa kawaida badala ya kujikita kwenye nishati ya mafuta, gesi na umeme.

Hivyo Waziri Makamba akasema, ataweka msisitizo sana kwenye nishati jadidifu ambayo ni ya kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya jua na upepo.

Lakini pamoja na kazi zinazoendelea sasa hivi, alisema ataangalia kikubwa kingine, kwamba atalenga kupunguza matumizi ya mkaa ili kuachana na matumizi ya mkaa hususan katika Jiji la Dar es Salaam.

Hiyo ni kwa sababu Dar es Salaam ndilo jiji nchini, linaloongoza kwa kupatiwa umeme, lakini pia linaongoza kwa matumizi makubwa ya mkaa.

Hivyo Waziri Makamba akawaelekeza wataalamu kuibua mradi wa namna ya kuachana na matumizi ya mkaa Dar es Salaam na kwa nchi nzima kiujumla, ili kulinda mazingira.

Kwa upande wa ujumbe wa Uingereza walikuwa na masuala ya uwekezaji katika miradi ya uzalishaji nishati ya umeme kutokana na nguvu ya jua na upepo, ambapo ulionesha nia ya kuwekeza katika maeneo hayo.

Hivyo, ubalozi wa Uingereza ukataka kujua Serikali ya Tanzania imejiandaaje na kama kuna fursa za kuwekeza ambapo Waziri wa Nishati, Makamba aliuambia kwamba fursa hizo zipo.

Aidha, ubalozi huo ukataka kujua, kuhusu Mpango Kabambe wa Nishati Tanzania unasemaje, ambapo Wizara ya Nishati imepanga ifikapo mwaka 2025 kuwe na megawati zisizopungua 700.

"Kwa sababu tunataka tuwe na megawati 350 kutokana na jua na 350 za upepo lakini kwa kuanzia, Wizara ya Nishati ilipanga kuanza na megawati 350 hadi ilipofika mwaka jana, za

# MAKAMBA AJA NA MWELEKEO MPYA NISHATI

jua zikiwa 150 na 200 za upepo," aliosema Waziri Makamba.

Aliongeza kuwa "kuanzia mwaka 2020 hadi 2025 tunatakiwa tufikishe megawati 700. Jua likizalisha megawati 350 huku 350 zikitokana na upepo na kuingizwa kwenye gridi ya Taifa," alisema Waziri wa Nishati akisisitiza kuwa huo ndio utakuwa mpango wake.

Pamoja na mambo mengine, Waziri Makamba aliwataka wataalamu wa Wizara yake kuandaa sera kuhusu tungamotaka (Biomas), kwa sababu imeonekana nchini asilimia 80 ya nishati inatokana na taka.

Kwa sasa Wizara ya Nishati haina sera ya tungamotaka , hivyo Waziri Makamba aliwaelekeza wataalamu kuiandaa ikionesha matumizi ya tungamotaka, na kwa maana hiyo isaidie kupunguza matumizi ya mkaa na kulinda mazingira.

Ujumbe huo wa Uingereza ulijielekeza pia katika suala la kuzalisha umeme kwa kutumia wazalishaji wadogo, ukitaka kujua Serikali imefikia hatua gani katika majadiliano kuhusu gharama za uwekezaji katika kuzalisha umeme kutokana na vyanzo vidogo.

Lakini huko nyuma, Serikali ilishatoa maelekezo kuhusu viwango vya bei kwa wazalishaji hao wa umeme, kutumia vyanzo vidogo, kutokana na kuwa na viwango tofauti vya bei, ambapo kila mzalishaji mdogo alitoza bei yake katika maeneo mbalimbali.

Mwaka jana Serikali ilitoa maelekezo kwa wazalishaji wadogo wote, kwamba watoze viwango vya bei sawa na vya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Ubalozi wa Uingereza ulilenga kuendelea kusaidia wazalishaji umeme wadogo, ili waendelee kuzalisha nishati hiyo na kuchangia kwenye uzalishaji wa nchi lakini wanashindwa kufanya hivyo, kwa sababu viwango vinavyotozwa vinashindwa kurudisha faida.

Kutokana na nia hiyo njema ya Uingereza, Waziri Makamba akaahidi kulipitia suala hilo vema na kulitolea uamuzi.

Kwa hatua hiyo, Uingereza ilionesha nia ya kuwekeza katika miradi ya nishati jadidifu, ambayo ni ya kuzalisha umeme wa jua na upepo na kuwa tayari kusaidia Tanzania katika eneo hilo.

Kupitia Balozi Concar, Uingereza ilisema inasubiri kujua kwamba Serikali ya Tanzania na hasa uongozi mpya wa Wizara ya Nishati umejiandaaje katika eneo hilo.

Waziri Makamba alisema kuanzia sasa ataelekeza nguvu katika nishati jadidifu, kwa sababu anaona huku kwingine hatua imeshapigwa sana na hivyo hapana sababu kila mara kuzungumzia gesi na maji.

Hivyo, ni wakati sasa kuzungumzia upepo na jua.



*Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza na Balozi wa Uingereza nchini, Donald Concar (hayupo pichani) alipomtembelea kwenye ofisi ndogo za Wizara ya Nishati, Dar es Salaam hivi karibuni. Kulia kwa Waziri ni Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali.*

# MAKAMBA AJA NA MWELEKEO MPYA NISHATI



*Waziri wa Nishati, January Makamba akiwa na mgeni wake, Balozi wa Uingereza nchini, Donald Concar alipomtembelea ofisini kwake hivi karibuni kwenye ofisi ndogo za Wizara ya Nishati Dar es Salaam*

Aliahidi kuja na mikakati ya kuhakikisha Tanzania inazalisha umeme wa jua na upepo.

Wizara ya Mishati ina Sera ya Nishati yaTaifa



*Waziri Januari Makamba akizungumza na Balozi wa Uingereza nchini, Donald Concar. Kushoto kwa Balozi ni Mshauri wa Balozi kuhusu Maendeleo ya Sekta Binafsi, Tom Ratsakatika.*

ya mwaka 2015 lakini imejumuisha nishati zote pamoja; yaani mafuta, gesi, tungamotaka na umeme wa kawaida.

Kwa hiyo Waziri Makamba anataka kwa kuwa tungamotaka mchango wake ni mkubwa kwa zaidi ya asilimia 80, ni bora kuwa na sera ya tungamotaka, ili kusimamia vizuri chanzo hicho cha umeme.

Lakini lingine ni kutaka matumizi ya LPG yafike sehemu zote. Kwani REA ni Rural Energy Agency kwa maana ya Wakala wa Nishati Vijijini na si Rural Electrification Agency yaani Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini.

Hivyo kama REA ni wakala wa nishati, basi ipo sababu ya kuhakikisha nishati zote zinasambazwa katika vijiji nchini si tu umeme peke yake, bali pia nishati ya umeme wa gesi na wa vyanzo vingine.

Hivyo, kwa sasa hivyo ndivyo vipaumbele vya Waziri Makamba.

# WATUMISHI WA TANESCO WATAKIWA KUJIANDAA KUIJENGA TANESCO MPYA





*Waziri wa Nishati, Mhe. January Yusuf Makamba, akizungumza na Watumishi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakati wa mkutano wake na Mameneja wa TANESCO wa Kanda, Mikoa na Wilaya, uliofanyika tarehe 26 Septemba, 2021 katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam Waziri Makamba amewataka watumishi hao kuwa tayari kupokea mabadiliko, kufanya kazi kwa bidii na weledi na kutoa ushirikiano mzuri kwa uongozi wa TANESCO na bodi mpya iliyoteuliwa ili kulijenga upya Shirika la TANESCO na kuliwezesha kufikia malengo yanayotarajiwa na Serikali.*

**Na Dorina G. Makaya – Dar-es-salaam.**

Watumishi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wamewatakiwa kuwa tayari kupokea mabadiliko, kufanya kazi kwa bidii na weledi na kutoa ushirikiano mzuri kwa uongozi wa TANESCO na bodi mpya iliyoteuliwa ili kulijenga upya Shirika la TANESCO na kuliwezesha kufikia malengo yanayotarajiwa na Serikali.

Rai hiyo imetolewa na Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba tarehe 26 Septemba, 2021 alipokuwa anazungumza na watumishi wa TANESCO kwenye mkutano wake na Mameneja wa TANESCO uliofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam.

Waziri Makamba amewaambia watumishi wa TANESCO, kuanzia sasa, hakutakuwa na uonevu kabisa kwenye Shirika la TANESCO na kuwa, wafanyakazi wajiweke tayari kufanya kazi kwa ushirikiano, bidii na maarifa ili kuongeza utendaji wenye tija.

Amesema, uteuzi uliofanywa wa viongozi wa juu wa Menejimenti ya TANESCO na Bodi, unatoa taswira na ishara namna ambavyo Serikali inataka shirika la TANESCO liongozwe.

Aidha, Waziri Makamba ameeleza



*Mameneja wa TANESCO wa Kanda, Mikoa na Wilaya, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Mhe. January Yusuf Makamba, alipokuwa akizungumza nao wakati wa mkutano wake na mameneja hao uliofanyika tarehe 26 Septemba, 2021 katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam.*

# WATUMISHI WA TANESCO WATAKIWA KUJIANDAA KUIJENGA TANESCO MPYA

kuwa, mkutano huo umelenga kufahamiana na kuutambulisha uongozi mpya kwa watumishi hao wa TANESCO na kuwa, uteuzi na utenguzi uliofanywa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan na ule uliofanywa na yeye Waziri wa Nishati, unamaanisha kuwa, Serikali inataka mapinduzi makubwa katika sekta ya umeme.

"Tunataka shirika letu liendeshwe kwa ufanisi, kibiashara, liwe shirika linalowajali watumishi wake, linalochangia kwenye maendeleo na ukuaji uchumi hapa nchini na linaloheshimika zaidi Afrika Mashariki. Tumewaletea uongozi mpya, bodi mpya na sasa tunaanza safari yenye mwelekeo mpya." Alisema Waziri Makamba.

Waziri Makamba aliongeza kuwa, Serikali haitavumilia wizi, dhuluma wala hujuma na inatarajia kiwango cha juu sana cha uadilifu na uchapa kazi na kuwa, hiyo ni ahadi inayopeana kati ya viongozi na Serikali.

Akizungumzia kuhusu mabadiliko yaliyofanyika hivi karibuni kwa uongozi wa TANESCO, Waziri Makamba amesema, ni uamuzi mgumu sana kumuondoa mtu kazini hasa mtu mwenye nafasi kubwa kama Mkurugenzi Mkuu, mtu wa manunuzi, mtu wa sheria, lakini ni uamuzi ambao ni



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, akizungumza na Watumishi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwenye mkutano wa Waziri wa Nishati na Mameneja wa TANESCO wa Kanda, Mikoa na Wilaya, uliofanyika tarehe 26 Septemba, 2021 katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam*
*Naibu Waziri Byabato, amewaambia watumishi wa TANESCO kuwa, anaamini bodi iliyoteuliwa itatoa ushauri utakaoiwezesha TANESCO kufikia malengo yanayotarajiwa.*



*Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO Bw. Omari Issa akizungumza na Watumishi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakati wa mkutano wa Waziri wa Nishati na Mameneja wa TANESCO wa Kanda, Mikoa na Wilaya, uliofanyika tarehe 26 Septemba, 2021 katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam*
*Bw. Issa, amemhakikishia Waziri Makamba kuwa, watahakikisha wanarudisha heshima ya Shirika la TANESCO na ufanisi kupitia ushirikiano wa watumishi na Uongozi wa Wizara ya Nishati.*

# WATUMISHI WA TANESCO WATAKIWA KUJIANDAA KUIJENGA TANESCO MPYA

wa lazima ili kufikia malengo.

"Na uamuzi huo tumeuchukua kwa sababu tunataka mambo yaende. Hawa walioondolewa wamefanya kazi mpaka walipotufikisha, na haina doa kwamba ni watu ambao ni wa ovyo ila tunataka mwelekeo mpya. Na tunahitaji timu mpya ambayo itatupeleka kule tunarajia. Alisema Waziri Makamba.

Waziri Makamba amewaambia watumishi hao wa TANESCO kuwa, Mwenendo mpya ni kuwa, atakayefanya kazi vizuri, ataonekana na atatunukiwa. "Tunaamini kwamba mabadiliko yaliyofanyika na mwelekeo mpya mmeupokea na mtautekeleza" alisema Waziri Makamba.

Akizungumza kwa nyakati tofauti katika kikao hicho, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amesema, bodi iliyoteuliwa ni muhimu sana kwa maendeleo ya shirika la TANESCO na kuwa Wizara ya Nishati inaitegemea sana bodi hiyo katika kutoa



*Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw. Maharage Chande, akizungumza na Mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wa Kanda, Mikoa na Wilaya wakati wa mkutano wa Waziri wa Nishati na Mameneja hao, uliofanyika tarehe 26 Septemba, 2021 katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam*
*Bw. Chande amewaomba watumishi wa TANESCO wampe ushirikiano ili kwa pamoja wafanye kazi kwa bidii wateja waweze kuongezeka na kuliwezesha shirika la TANESCO kupata faida.*

ushauri utakaoiwezesha TANESCO kufikia malengo yanayotarajiwa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO Bw. Maharage Chande amewaambia watumishi hao wa TANESCO kuwa, malipo yatatokana na utendaji. Kama mtumishi anafanya kazi vizuri apewe aneemeke na mtumishi asiyefanya kazi vizuri afundishwe, na iwapo baada ya kufundishwa mtumishi bado hafanyi vizuri basi mtumishi huyo atakuwa hafai.

Bw. Chande amesema, maamuzi magumu hayawezi kufanikiwa bila kuwa na ushirikiano wa pamoja baina ya watumishi na viongozi na kuwataka watumishi wa TANESCO kwa pamoja washirikiane kuyatafuta yaliyo mazuri na pia washirikiane kuyakataa mabaya.

"Malipo kutokana na utendaji, ushirikishwaji wa wafanyakazi, motisha kwa wafanyakazi, uendelezaji wa watumishi kitaaluma, mpango mzuri wa kurithisha vyeo watumishi, ndiyo yatakayopewa uzito wa juu na yatafanyika kwa haraka sana." Amesema Chande.

Aidha, Bw. Chande amewatahadharisha watumishi hao wa TANESCO kuwa, wakati wa kuanza safari ya kuijenga TANESCO mpya, watakutana na changamoto na kuwataka wawe jasiri katika kusonga mbele.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu huyo wa TANESCO amesema, mara baada ya kikao hicho, atakutana na Mameneja hao wa TANESCO ili kutoa dira na mwelekeo wa shirika wenye lengo la kuifanya TANESCO kuwa shirika bora si tu kwa Afrika

# WATUMISHI WA TANESCO WATAKIWA KUJIANDAA KUIJENGA TANESCO MPYA



*Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga akimkaribisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Leonard Masanja (Hayumo Pichani) ili amkaribishe Waziri wa Nishati Mhe. January Yusuf Makamba kuzungumza na Mameneja wa TANESCO wa Kanda, Mikoa na Wilaya, katika mkutano uliofanyika tarehe 26 Septemba, 2021 katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam*

Mashariki bali katika bara la Afrika.

Naye mwenyekiti wa bodi ya TANESCO Bw. Omari Issa amesema, mabadiliko yanayotarajiwa kwa TANESCO yatafanywa na watumishi wa TANESCO wenyewe. Na kuwa, kipaumbele cha kwanza ni Rasilimali watu na kusisitiza kuwa kila mtumishi wa TANESCO awe tayari kubadilika ili kuyafikia malengo yaliyowekwa na Serikali kwa Shirika la TANESCO.

Amewaomba watumishi wa TANESCO waiunge mkono bodi ya TANESCO na kuyakubali mabadiliko ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Bw. Issa amemuomba Waziri wa Nishati kufikisha salaam zake kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, kwa kumuamini na kumteua kuiongoza bodi ya TANESCO na kuahidi kufanya kazi hiyo kwa uaminifu mkubwa na kwa kujituma.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, mameneja wa Kanda – TANESCO wamempongeza Waziri Makamba kwa uteuzi na kwa hotuba nzuri aliyoitoa kwa watumishi wa TANESCO yenye matumaini ya kuijenga kiupya TANESCO kwa lengo la kuongeza ufanisi na utendaji wenye tija.

Nae Meneja Mwandamizi wa Rasilimali watu Fransis Sangunaa, akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wa TANESCO, amesema, watumishi wa TANESCO watatoa ushirikiano mkubwa na wa kutosha ili kuyafikia malengo yale ambayo Serikali inatarajia kuyafikia kupitia shirika la TANESCO.

Akitoa neno la shukrani katika mkutano huo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, amewapongeza viongozi walioteuliwa na kuwashukuru viongozi hao kwa kushiriki katika kikao hicho muhimu.

Vile vile kwa niaba ya watumishi wote wa Wizara ya Nishati, amemshukuru Waziri wa Nishati kwa muongozo alioutoa na kuahidi kuwa viongozi wa Wizara ya Nishati pamoja na watumishi, wako tayari kutoa ushirikiano ili kuwezesha mapinduzi ya Nishati kwa ajili ya maendeleo makubwa zaidi.

Mkutano huo, umehudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Leonard Masanja, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Felchesmi Mramba, Kamishna wa Petrol na Gesi, Michael Mjinja, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati, Ziana Mlawa na mameneja wa TANESCO nchini.

# WATUMISHI WA TANESCO WATAKIWA KUJIANDAA KUIJENGA TANESCO MPYA













*Habari katika picha wakati wa Mkutano Waziri wa Nishati na Mameneja wa TANESCO wa Kanda, Mikoa na Wilaya, uliofanyika tarehe 26 Septemba, 2021 katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam*

# WATAALAMU NISHATI WAPEWA MAAGIZO MRADI WA EACOP

**Na Dorina G. Makaya & Janeth Mesomapya**

Waziri wa Nishati, Mh. January Yusuf Makamba, amewaagiza wataalamu wa Wizara ya Nishati kuunda timu itakayojumuisha sekretarieti za mikoa minane ambapo utapita mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) ili kutengeneza maelezo mahususi ya mikoa hiyo yatakayofanikisha unufaikaji wa fursa zitokanazo na utekelezaji wa mradi huo.

Waziri Makamba ameyasema hayo tarehe Septemba 28, 2021 katika siku ya pili ya semina kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa hiyo iliyofanyika jijini Tanga. Semina hiyo ililenga kubainisha fursa zitokanazo na mradi huo wa bomba la mafuta.

Ameelekeza kuwa maelezo hayo mahususi yatoe taarifa kamili kuhusu mahitaji kwenye mikoa hiyo katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi, maandalizi wanayotakiwa kuyafanya ili kukidhi mahitaji husika, thamani ya kazi kiuchumi, na mchanganuo wa fursa



*Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba akizungumza na Waandishi wa Habari mara baada ya kumaliza siku ya pili ya semina kuhusu fursa zitakazopatikana kutokana na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga kwa wakuu wa mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane itakayopitiwa na mradi, tarehe 28 Septemba, 2021.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akifuatilia kwa makini maoni yaliyokuwa yakitolewa na washiriki wa semina kwa Wakuu wa mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane ambayo itapitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga, tarehe 28 Septemba, 2021. Kushoto kwa Naibu Waziri Byabato ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Mhe. Naghenjwa Kaboyoka na kulia kwake ni Makamu mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Mhe. Japhet Hasunga.*



*Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe. Adam Malima (wa kwanza kulia) akitoa mchango wake kuhusu mada zilizowasilishwa wakati wa semina kwa Wakuu wa mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa minane itakayopitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga wakati wa semina kuhusu fursa zitakazopatikana kutokana na Mradi huo, inayoendelea jijini Tanga tarehe 28 Septemba, 2021.*

zitakazopatikana kulingana na mikoa hiyo na jiografia zake.

"Baada ya kupatikana maelezo hayo, iangaliwe namna bora ya kuwajengea uwezo wananchi wa mikoa husika ili wawe na uwezo wa kufanya kazi na kunufaika na fursa hizo, lengo likiwa kuwapa taarifa sahihi juu ya fursa za mradi ili wawe na mategemeo halisia" aliongeza.

Aidha, Waziri Makamba amewaagiza wasimamizi wa mradi huo, kuhakikisha Mpango wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) unalenga kunufaisha jamii zinazozunguka mradi ili manufaa halisi yaonekane pindi mradi unapofikia ukomo.

Kwa upande wa kanzidata maalumu ya watoa huduma inayoendeshwa na

# WATAALAMU NISHATI WAPEWA MAAGIZO MRADI WA EACOP



*Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) Dkt. James Mataragio (aliyesimama) akitoa maelezo mafupi kuhusu michango iliyotolewa na washiriki wa semina ya Wakuu wa mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane itakayopitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga, tarehe 28 Septemba, 2021*

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Waziri Makamba ameagiza kuwa, ufahamu wa kutosha utolewe kwa wananchi wa jinsi ya kujisajili kwenye kanzidata hiyo, ili watoa huduma wengi zaidi wawe sehemu ya jukwaa hilo.

Naye Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato alieleza kuwa, ili fursa za mradi huu zinufaishe kwanza jamii zinazopitiwa na bomba, serikali inaandaa mikakati ya kuhakikisha fursa hizo zinabaki ndani ya mikoa husika na kunufaisha watu wake.

"Tutaenda pia kwenye mikoa husika kuwaelezea wananchi fursa zilizopo kwenye mikoa yao kwa mchanganuo mzuri, ili wajiandae kuzichangamkia," aliongeza. Naibu Waziri Byabato.



*Afisa kutoka EWURA Kenneth Kaganga, akitoa wasilisho kwa Wakuu wa mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane kuhusu ushiriki wa Watanzania katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga, tarehe 28 Septemba, 2021*



*Washiriki wa Semina wakifuatia kwa makini michango iliyokuwa inatolewa wakati wa semina ya Wakuu wa mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane itakayopitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga, tarehe 28 Septemba, 2021*

# NAIBU WAZIRI NISHATI AHITIMISHA SEMINA FURSA ZA EACOP KWA VIONGOZI



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza na waandishi wa Habari mara baada ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane itakayopitiwa na bomba la mafuta kuwasili katika eneo la Chongoleani Tanga, tarehe 29 Septemba, 2021 mahali ambapo bandari itajengwa. Kushoto kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe. Adam Malima.*

**Na Dorina Makaya & Janeth Mesomapya**

Naibu Waziri wa Nishati Wakili Stephen Byabato ameongoza timu ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane (8) ambapo utapita mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) na baadhi ya viongozi wa serikali na taasisi za umma kufanya ziara katika eneo utakapoishia mradi huo Chongoleani, jijini Tanga.



*Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe. Adam Malima (wa kwanza kushoto), akizungumza na waandishi wa Habari mara baada ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane itakayopitiwa na bomba la mafuta kuwasili katika eneo la Chongoleani Tanga, tarehe 29 Septemba, 2021 mahali ambapo bandari itajengwa. Kulia kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato*

Katika ziara hiyo, Wakili Byabato ameeleza kuwa serikali imejipanga kuhakikisha manufaa yatakayotokana na mradi huo yanawanufaisha kwanza wakazi wa maeneo ambayo bomba hilo litapita.

"Tunatambua kuwa mradi huu utalinufaisha taifa kiuchumi lakini tunahitaji uanze ngazi ya chini kabisa ya wananchi ambao maeneo yao yatapitiwa na bomba hili, na hii ndio maana halisi ya ushirikishwaji wa

# NAIBU WAZIRI NISHATI AHITIMISHA SEMINA FURSA ZA EACOP KWA VIONGOZI



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akiangalia jiwe la msingi lililowekwa eneo la Chongoleani Tanga mahali ambapo bandari itajengwa wakati Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane itakayopitiwa na bomba la mafuta walipotembelea eneo hilo tarehe 29 Septemba, 2021*

wazawa katika miradi ya maendeleo," aliongeza.

Aliongeza kuwa kwa kutekeleza hilo, Waziri wa Nishati, Mh. January Yusuf Makamba amewaagiza wataalamu wa Wizara ya Nishati kushirikiana na sekretarieti za mikoa hiyo minane kutengeneza maelezo mahususi ya mikoa hiyo yatakayofanikisha unufaikaji wa fursa zitokanazo na utekelezaji wa mradi huo.

Naibu Waziri Byabato alihitimisha semina hiyo maalumu ya siku tatu iliyoandaliwa kwa lengo la kutoa uelewa wa mradi na fursa zitakazotokana na utekelezaji wake kwa viongozi hao.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mh. Adam Malima alisema kwamba mradi huu utavutia fursa nyingi zaidi za uwekezaji nchini kupitia bandari ya Tanga, hivyo ni vyema wananchi hususani wa mkoa wa Tanga wakajiandaa ili kuchangamkia fursa hizo.



*Mkuu wa Mkoa wa Singida Dkt. Binilith Mahenge, akizungumza na waandishi wa Habari wakati Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane itakayopitiwa na bomba la mafuta walipotembelea eneo hilo la Chongoleani Tanga tarehe 29 Septemba, 2021 mahali ambapo bandari itajengwa. Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*



*Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Tanga, Henry Shekifu, akizungumza na Waandishi wa Habari wakati Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane itakayopitiwa na bomba la mafuta walipotembelea eneo la Chongoleani Tanga tarehe 29 Septemba, 2021.*

# NAIBU WAZIRI NISHATI AHITIMISHA SEMINA FURSA ZA EACOP KWA VIONGOZI



*Mratibu wa Mradi wa Bomba la Mafuta Asiad Mrutu, akizungumza na Waandishi wa Habari tarehe 29 Septemba, 2021 wakati Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa minane itakayopitiwa na bomba la mafuta walipotembelea eneo la Chongoleani Tanga.*









# WAZIRI MAKAMBA AKUTANA NA TUICO -TANESCO



*Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba (Mb.) akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Majadiliano TUICO -TANESCO (Hawapo pichani) wakati wa kikao kilichofanyika leo tarehe 22 Septemba, 2021 kwenye ukumbi wa mikutano wa ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar-es-salaam.*

Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (Mb.) tarehe 22 Septemba, 2021 alikutana na kamati ya Majadiliano ya Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) –TANESCO kwenye ukumbi wa mikutano wa ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar-es-salaam kwa lengo la kufahamiana na kupata maoni ya wafanyakazi namna ya kuboresha utendaji wa TANESCO.

Waziri Makamba alipokea maoni mbalimbali kutoka kwa viongozi hao wa chama cha wafanyakazi (TUICO) -TANESCO na kuahidi kuyafanyia kazi ipasavyo maoni yaliyotolewa ili kuhakikisha kiwango cha utendaji kazi wa TANESCO kinaongezeka na maslahi muhimu ya wafanyakazi yanazingatiwa.



*Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba (Mb.) akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Majadiliano TUICO-TANESCO wakati wa kikao kilichofanyika leo tarehe 22 Septemba, 2021 kwenye ukumbi wa mikutano wa ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar-es-salaam.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Leonard Masanja, akizungumza wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba (Mb.) na wajumbe wa Kamati ya Majadiliano TUICO -TANESCO (Hawapo pichani) kilichofanyika leo tarehe 22 Septemba, 2021 kwenye ukumbi wa mikutano wa ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar-es-salaam.*

# WAZIRI MAKAMBA AKUTANA NA TUICO -TANESCO



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Leonard Masanja (wa kwanza kulia) na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Kheri Mahimbali (wa pili kutoka kulia) wakifuatilia kwa makini, wakati Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu wa Wizara ya Nishati, Bi. Ziana Mlawa akizungumza wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba (Mb.) na wajumbe wa Kamati ya Majadiliano TUICO-TANESCO (Hawapo pichani) kilichofanyika leo tarehe 22 Septemba, 2021 kwenye ukumbi wa mikutano wa ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar-es-salaam.*



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Kheri Mahimbali (wa kwanza kushoto) akifuatilia kwa makini, wakati Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu wa Wizara ya Nishati, Bi. Ziana Mlawa akizungumza wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba (Mb.) na wajumbe wa Kamati ya Majadiliano TUICO-TANESCO (Hawapo pichani) kilichofanyika leo tarehe 22 Septemba, 2021 kwenye ukumbi wa mikutano wa ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar-es-salaam*





*Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba (Mb.) akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Majadiliano TUICO-TANESCO (Hawapo pichani) wakati wa kikao kilichofanyika leo tarehe 22 Septemba, 2021 kwenye ukumbi wa mikutano wa ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar-es-salaam.*





*Wajumbe wa Kamati ya Majadiliano TUICO-TANESCO wakimsikiliza Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba (Mb.) wakati wa kikao kilichofanyika leo tarehe 22 Septemba, 2021 kwenye ukumbi wa mikutano wa ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar-es-salaam.*

# TANESCO KUWA SHIRIKA BORA AFRIKA MASHARIKI



*Kaimu Mkurungenzi Mtendaji usafirishaji Muhandisi Abubakari Issa akimuelezea Waziri wa Nishati Mhe. Januari Makamba njinsi kituo cha kupokea na kupoza umemecha ubungo kinavyo pokea na kusambaza umeme.*

Waziri wa Nishati, January Makamba wakati akikagua kituo cha kudhibiti mifumo ya umeme wa Gridi ya Taifa, leo Septemba 17, 2021 amesema atahakikisha TANESCO inakuwa Shirika bora Afrika Mashariki.

Aidha amewataka watendaji wa Shirika kujianda kwa mabadiliko makubwa yenye tija yatakayo saidia kuimarisha Shirika ili kuongeza tija na ufanisi.

Mhe. Makamba ameagiza TANESCO kuhakikisha wanatatua matatizo ya kukatika kwa umeme kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini, ambapo ametoa wiki mbili kwa wataalamu kuhakikisha wanatatua tatizo hilo kwenye maeneo mbalimbali.

Lengo la Mhe. Makamba kufika kwenye kituo cha kudhibiti mifumo ya umeme wa Grid ya Taifa kilichopo ubungo Dar es salaam, ni kujifunza na kuelewa kuhusu mfumo mzima wa Grid ya Taifa.

Mhe. Makamba amesema Shirika lina mambo mengi ya kufanya kama uwekezaji mbalimbali na kuongeza wateja Nchi nzima ili kuweza kufikia adhima yake yakua shirika bora Afrika Mashariki.



*Waziri wa Nishati, Mhe. Januari Makamba akitoa maelekezo kwa viongozi wa TANESCO wakati alivyo tembelea kitengo cha mfumo wa udhibiti umeme( Grid control center).*

# Makamba aanza kazi rasmi Wizara ya Nishati

**Zuena Msuya na Hafsa Omari, Dodoma**

Waziri wa Nishati, January Makamba, ameanza kazi rasmi katika wizara hiyo kwa kuwataka watendaji wa wizara hiyo pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo kufanya kazi kwa weledi wa uaminifu na uadilifu kwa maslahi mapana ya Taifa.

Amesema hayo wakati akizungumza na Uongozi wa Wizara hiyo pamoja Taasisi zilizo chini yake, mara baada ya kushika wadhifa huo na kuwasili katika ofisi za Wizara hiyo zilizopo katika Mji wa Magufuli Mtumba, Septemba 13, 2021.



*Waziri wa Nishati, January Makamba (aliyeshika Ua) baada ya kuwasili katika ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mji wa Magufuli Mtumba tayari kuanza majukumu yake mara baada ya kuapishwa kushika wadhifa huo, Septemba 13, 2021, wa pili kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*



*Waziri wa Nishati, January Makamba akisalimiana na Wakuu wa Taasisi zilizochini ya Wizara ya Nishati pamoja na Viongozi Waandamizi wa Wizara hiyo mara baada ya Waziri huyo kuapishwa kushika wadhifa huo na kuwasili wizarani hapo, Septemba 13,2021.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja(aliyesimama )kumkaribisha Waziri wa Nishati, January Makamba katika kikao cha Waziri huyo na Uongozi wa Wizara na Taasisi zilizochini ya Wizara mara baada ya Waziri huyo kuapishwa kushika wadhifa huo na kuwasili wizarani hapo, Septemba 13,2021.*

# Makamba aanza kazi rasmi Wizara ya Nishati

Aliwaeleza watumishi hao kuwa anahitaji kuona matokeo chanja katika utendaji kazi pamoja na kutekeleza majukumu yao kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Leonard Masanja, Naibu Katibu Mkuu, Kheri Mahimbali, Viongozi Waandamizi wa wizara pamoja na Wakuu wa Taasisi zilizochini ya Wizara hiyo.

Aidha, aliwataka watumishi hao kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuweza kusukuma mbele Sekta ya Nishati kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi na kukuza uchumi wa Taifa kwakuwa sekta hiyo ni muhimili muhimu katika kukuza uchumi wa nchi.

Sambamba na hilo amezitaka Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo,ambazo ni Shirika la Umeme Tanzania( TANESCO), Wakala wa Nishati Vijijini( REA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji( Ewura), Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja( PBPA) Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania( TPDC) na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Mafuta( PURA),kuhakikisha zinafanya kazi kwa kuzingatia maslahi ya nchi na watanzania kwa jumla.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato alitoa pongezi kwa Waziri Nishati kwa kuaminiwa na kuteuliwa kushika nafasi hiyo na Rais Mhe. Samia Suluhu Hasani na kwamba watumishi wa Wizara wamempokea kwa moyo mkunjufu.

Vilevile alimuhakikishia Waziri Makamba, kuwa watumishi wa Wizara pamoja na Tasisi zilizo chini ya wizara hiyo zitatoa ushirikiano mkubwa wa kiutendaji katika kuhakikisha sekta hiyo inasonga mbele na kunufaisha Taifa na watanzania kwa jumla.



*Waziri wa Nishati, January Makamba (katikati mstari wa mbele),akiwa katika picha ya pamoja viongozi waandamizi wa Wizara hiyo na Taasisi zilizochini ya Wizara hiyo baada ya kumaliza kikao chake na uongozi huo baada ya kuapishwa kushika wdhifa huo, Septemba 13,2021.*

# WAZIRI MAKAMBA AKUTANA NA UONGOZI WA EQUINOR NA SHELL



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (wa kwanza kushoto) akimsikiliza Makamu wa Rais na Mwenyekiti Mkazi wa kampuni ya Shell Tanzania, Jared Keuhl (hayumo pichani) wakati wa kikao kilichofanyika leo tarehe 24 Septemba, 2021 katika ukumbi wa mikutano wa ofisi ndogo za Wizara ya Nishati jijini Dar-es-salam. Kulia kwake ni Naibu waziri wa Wizara ya Nishati, Wakili Stephen Byabato na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali.*

**Na Dorina G. Makaya na Janeth Mesomapya – Dar-es-Salaam**

Waziri wa Nishati Mhe. January Yusuf Makamba, tarehe 24 Septemba, 2021 alikutana na uongozi wa kampuni za Equinor na Shell kwa lengo la kufahamiana na kufanya mazungumzo mafupi kuhusu kuanza kwa majadiliano ya mkataba wa nchi hodhi (HGA) wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG).

Katika kikao hicho Waziri Makamba, ameuhakikishia uongozi wa kampuni za Equinor na Shell kuwa, Serikali ya Tanzania iko tayari kuanza majadiliano ya mkataba wa nchi hodhi (HGA) ambayo yanatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwezi Octoba, 2021.

Aidha, wadau hao wameihakikishia Serikali kwamba wako tayari kwa ajili ya kuanza majadiliano na kuwa timu yao itakayoongoza majadiliano hayo tayari iko jijini Dar-es-Salaam.

Kwa upande wa Wizara ya Nishati, baadhi ya viongozi waliohudhuria kikao hicho ni pamoja na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, Kamishna wa Petroli na Gesi Adam Zuberi, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) Dkt. James Mataragio na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) Mha. Charles Sangweni.



*Makamu wa Rais na Mwenyekiti Mkazi wa kampuni ya Shell Tanzania, Jared Keuhl akizungumza na Waziri wa Nishati (Hayumo pichani) wakati wa kikao kilichofanyika leo tarehe 24 Septemba, 2021 katika ukumbi wa mikutano wa ofisi ndogo za Wizara ya Nishati jijini Dar-es-salam. Kushoto kwake ni Makamu wa Rais na Mwenyekiti Mkazi, Equinor Tanzania AS, Unni Merethe Skolstad Fjaer.*

# WAZIRI MAKAMBA AKUTANA NA UONGOZI WA EQUINOR NA SHELL











# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI













***Fika Ofisi ya Mawasiliano,***
**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi** +255-26-2320148

***www.nishati.go.tz***
***Wizara ya Nishati***
***@Nishati2017***
***wizara_ya_nishati_tanzania***
***Wizara ya Nishati***